**NA. 04: TOLEO LA TAKWIMU ZA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII - ZANZIBAR KWA MWEZI WA JANUARI HADI MACHI, 2025**

### 1.0 Utangulizi
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa utekelezaji wa majukumu yake iliyojipangia katika kuimarisha takwimu za Matukio ya Kijamii. Miongoni mwa takwimu hizo ni takwimu za Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka.

Toleo la robo ya kwanza ya mwaka 2025 (Jan-Machi), linatoa muhtasari wa takwimu za Matukio ya kijamii. Takwimu hizi zinatolewa kwa kulinganisha kijiografia (Wilaya) na kijinsia. Takwimu za Matukio ya Kijamii hutoa taarifa za idadi ya matukio ya kijamii yaliyosajiliwa na Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar.

### 2.0 Lengo
Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za Usajili wa Matukio ya Kijamii za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu katika kupanga maendeleo ya kijamii, kupima mafanikio ya Sera za Afya na kutambua changamoto za kijamii. Aidha, takwimu za matukio ya Kijamii husaidia katika kutathimini maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi, pia hutoa mwongozo muhimu kwa watafiti, serikali, na mashirika ya maendeleo katika kufanya tathimini na maamuzi sahihi kwa jamii. Toleo hili linawasilisha takwimu zifuatazo.

## 2.1 Usajili wa Vizazi hai
Jumla ya Vizazi hai 11,618 vimeripotiwa kusajiliwa kwa kipindi cha Januari hadi Machi, 2025, ambapo 5,739 (49.4%) ni wanaume na wanawake 5,879 (50.6%), usajili unaonesha kuwa uwiano wa jinsi ni wanaume 98 kwa kila wanawake 100. Aidha usajili umekuwa ukibadilika (kuongezeka na kupungua) kwa mwezi wa Januari 2025 vizazi 4,545 (39.1%) na kupungua hadi vizazi 3,281(28.2%) kwa mwezi wa Febuari 2025 na kuongezeka kwa mwezi wa March 2025, hadi kufikia 3,792 (32.6%) (Jadweli Na. 1).

Usajili unaonesha kuwa kipindi cha Januari-Machi 2025, Wilaya ya Mjini imeripotiwa kusajili vizazi hai 2,623 (22.6%) ikifuatia na Wilaya ya Micheweni na Wilaya ya Wete ambazo zimeripoti kusajili vizazi asilimia 12.8 (1,491) na asilimia 11.0% (1,282) mtawalia. Wilaya ya Kaskazini "B" imeripotiwa kusajili vizazi hai kidogo asilimia 2.1% (243) ukilinganisha na Wilaya nyingine.

**Jadweli Na. 1: Usajili wa Vizazi hai kwa Jinsi na Wilaya, Januari-Machi 2025**

| Wilaya | Januari-2025 | | | Febuari-2025 | | | Machi-2025 | | | Jan-Machi, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 138 | 158 | 296 | 155 | 215 | 370 | 191 | 230 | 421 | 484 | 603 | 1,087 |
| Kaskazini B | 59 | 76 | 135 | 27 | 22 | 49 | 29 | 30 | 59 | 115 | 128 | 243 |
| Kati | 90 | 116 | 206 | 69 | 76 | 145 | 64 | 76 | 140 | 223 | 268 | 491 |
| Kusini | 75 | 81 | 156 | 66 | 67 | 133 | 82 | 79 | 161 | 223 | 227 | 450 |
| Mjini | 488 | 440 | 928 | 445 | 377 | 822 | 435 | 438 | 873 | 1,368 | 1,255 | 2,623 |
| Magharibi A | 221 | 187 | 408 | 141 | 174 | 315 | 112 | 100 | 212 | 474 | 461 | 935 |
| Magharibi B | 200 | 215 | 415 | 81 | 94 | 175 | 210 | 175 | 385 | 491 | 484 | 975 |
| Micheweni | 337 | 335 | 672 | 191 | 156 | 347 | 239 | 233 | 472 | 767 | 724 | 1,491 |
| Chakechake | 117 | 127 | 244 | 164 | 215 | 379 | 140 | 193 | 333 | 421 | 535 | 956 |
| Mkoani | 310 | 329 | 639 | 103 | 125 | 228 | 128 | 90 | 218 | 541 | 544 | 1,085 |
| Wete | 215 | 231 | 446 | 154 | 164 | 318 | 263 | 255 | 518 | 632 | 650 | 1,282 |
| **Jumla** | 2,250 | 2,295 | 4,545 | 1,596 | 1,685 | 3,281 | 1,893 | 1,899 | 3,792 | 5,739 | 5,879 | 11,618 |

### 2.1.1 Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi Hai, Oktoba- Disemba 2024 na Januari-Machi 2025

Katika kipindi cha Oktoba - Disemba 2024, usajili wa vizazi hai ulikuwa wa kiwango cha chini kwa jumla ya vizazi 1,287, huku wanaume wakiwa 760 na wanawake 527. Wilaya ya Mjini ndiyo iliyosajili vizazi vingi zaidi (633), ikifuatiwa na Magharibi B (166), huku Wilaya ya Kusini na Kaskazini B zikisajili idadi ndogo (chini ya vizazi 20 kwa Wilaya).

Kwa upande wa Januari - Machi 2025, kulikuwa na ongezeko la usajili wa vizazi hai, ambapo jumla ya vizazi 11,618 vilisajiliwa, hii sawa na ongezeko la usajili wa vizazi 10,331 (800%) ikilinganishwa na robo mwaka ya mwisho wa mwaka 2024 (Oktoba-Disemba 2024). Ongezeko zaidi linaonekana katika wilaya ya Mjini ikiwa imesajili jumla ya vizazi 2,623, Micheweni jumla ya vizazi 1,491, na wilaya ya Wete imesajili jumla ya vizazi 1,282. Ongezeko hili linato ishara ya jitihada zinazowekwa katika huhamasishaji wa usajili wa matukio ya kijamii.

Kwa ujumla, tofauti kubwa kati ya vipindi hivi viwili inaashiria uimarishaji wa upatikanaji wa huduma za usajili wa vizazi hai. Aidha, ongezeko hili linaweza kuwa ni matokeo ya uhamasishaji wa jamii uliofanyika mwanzoni mwa mwaka 2025 juu ya umuhimu wa usajili wa vizazi kwa ajili ya huduma za jamii (elimu na afya) na kisheria (Vitambulisho ZanID na NIDA).

**Jadweli Na. 2: Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi hai kwa Jinsi na Wilaya, Okt- Dis 2024 na Jan-Machi 2025**

| Wilaya | Oktoba-Disemba 2024 | | | Jan-Machi, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 75 | 55 | 130 | 484 | 603 | 1,087 |
| Kaskazini B | 12 | 3 | 15 | 115 | 128 | 243 |
| Kati | 17 | 16 | 33 | 223 | 268 | 491 |
| Kusini | 7 | 10 | 17 | 223 | 227 | 450 |
| Mjini | 352 | 281 | 633 | 1,368 | 1,255 | 2,623 |
| Magharibi A | 26 | 24 | 50 | 474 | 461 | 935 |
| Magharibi B | 92 | 74 | 166 | 491 | 484 | 975 |
| Micheweni | 27 | 8 | 35 | 767 | 724 | 1,491 |
| Wete | 70 | 19 | 89 | 632 | 650 | 1,282 |
| Chakechake | 46 | 18 | 64 | 421 | 535 | 956 |
| Mkoani | 36 | 19 | 55 | 541 | 544 | 1,085 |
| **Jumla** | **760** | **527** | **1,287** | **5,739** | **5,879** | **11,618** |

## 2.1.2 Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi Hai, Januari- Machi, 2024 na Januari-Machi, 2025

Katika kipindi cha Januari - March 2024, usajili wa vizazi hai ulikuwa wa kiwango cha juu kwa jumla ya vizazi 13,282, huku wanaume wakiwa 6,410 na wanawake 6,872. Kwa upande wa Januari - Machi 2025, usajili wa vizazi hai, ulishuka ikilinganishwa na robo mwaka kama hiyo katika mwaka 2024 ambapo jumla ya vizazi 11,618 vilisajiliwa, hii sawa na upungufu wa vizazi 1,664.

Upungufu huo zaidi umeonekana katika wilaya ya Mjini ambapo usajili umeshuka kutoka vizazi 3,466 kwa Januari-Machi, 2024 na kushuka hadi vizazi 2,623 kwa Januari-Machi, 2025.

**Jadweli Na. 3: Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi hai kwa Jinsi na Wilaya, Jan- Machi 2024 na Jan-Machi 2025**

| Wilaya | Jan-Machi, 2024 | | | Jan-Machi, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 628 | 669 | 1,297 | 484 | 603 | 1,087 |
| Kaskazini B | 189 | 212 | 401 | 115 | 128 | 243 |
| Kati | 435 | 524 | 959 | 223 | 268 | 491 |
| Kusini | 191 | 168 | 359 | 223 | 227 | 450 |
| Mjini | 1,644 | 1,822 | 3,466 | 1,368 | 1,255 | 2,623 |
| Magharibi A | 443 | 479 | 922 | 474 | 461 | 935 |
| Magharibi B | 395 | 357 | 752 | 491 | 484 | 975 |
| Micheweni | 570 | 616 | 1,186 | 767 | 724 | 1,491 |
| Chakechake | 707 | 676 | 1383 | 421 | 535 | 956 |
| Mkoani | 545 | 575 | 1,120 | 541 | 544 | 1,085 |
| Wete | 663 | 774 | 1,437 | 632 | 650 | 1,282 |
| **Jumla** | 6,410 | 6,872 | 13,282 | 5,739 | 5,879 | 11,618 |

## 2.2 Usajili wa Vifo

Jumla ya Vifo 668 vimesajiliwa kwa kipindi cha miezi mitatu (Januari – Machi, 2025), ambapo 384 (57.5 %) ni wanaume na 284 (42.5%) wanawake. Aidha, uwiano wa vifo vilivyosajiliwa kwa jinsi ni wanaume 135 kwa wanawake 100, hii inaonesha kuwa usajili wa vifo kwa wanaume ni mkubwa ukilinganisha na wanawake (Jadweli Na.2). Usajili wa vifo umekua ukibadilika (kuongezeka na kupungua), ambapo kwa mwezi wa Januari 2025 jumla ya vifo 236 (35.3%) vimesajiliwa na kupungua hadi kufikia vifo 165 (24.7%) mwezi Febuari 2025 na kuongezeka hadi kufikia vifo 267 (40.0%) mwezi wa Machi 2025.

Katika kipindi cha Januari -Machi 2025, Wilaya ya Mjini imesajili jumla ya vifo 211 (31.6%), ikifuatiwa na Wilaya ya Magharibi "B" iliyosajili vifo 125 (18.7%) ya vifo. Aidha Wilaya ya Kaskazini "B" usajili wa vifo ni mdogo kwa kipindi cha Januari – Machi 2025 (15) ukilinganishwa na wilaya nyingine (Jadweli 3).

**Jadweli Na. 4: Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Januari-Machi 2025**

| Wilaya | Januari-2025 | | | Febuari-2025 | | | Machi-2025 | | | Jan-Machi, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 5 | 4 | 9 | 9 | 1 | 10 | 12 | 7 | 19 | 26 | 12 | 38 |
| Kaskazini B | 2 | 2 | 4 | 3 | 3 | 6 | 3 | 2 | 5 | 8 | 7 | 15 |
| Kati | 11 | 3 | 14 | 5 | 3 | 8 | 4 | 4 | 8 | 20 | 10 | 30 |
| Kusini | 11 | 4 | 15 | 0 | 7 | 7 | 4 | 5 | 9 | 15 | 16 | 31 |
| Mjini | 35 | 28 | 63 | 31 | 25 | 56 | 43 | 49 | 92 | 109 | 102 | 211 |
| Magharibi A | 14 | 6 | 20 | 7 | 4 | 11 | 4 | 9 | 13 | 25 | 19 | 44 |
| Magharibi B | 37 | 19 | 56 | 8 | 10 | 18 | 23 | 28 | 51 | 68 | 57 | 125 |
| Micheweni | 7 | 2 | 9 | 13 | 5 | 18 | 5 | 2 | 7 | 25 | 9 | 34 |
| Chakechake | 10 | 5 | 15 | 9 | 6 | 15 | 11 | 7 | 18 | 30 | 18 | 48 |
| Mkoani | 6 | 3 | 9 | 7 | 4 | 11 | 15 | 6 | 21 | 28 | 13 | 41 |
| Wete | 13 | 9 | 22 | 1 | 4 | 5 | 16 | 8 | 24 | 30 | 21 | 51 |
| Jumla | 151 | 85 | 236 | 93 | 72 | 165 | 140 | 127 | 267 | 384 | 284 | 668 |

### 2.2.1 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Okt-Dec, 2024 na Jan-Machi 2025

Katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba 2024, jumla ya vifo vilivyosajiliwa ni 1,287, ambapo wanaume walikuwa 760 (59.1%) na wanawake 527 (40.9%). Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya vifo vilivyosajiliwa ambavyo ni 633 (49.2%), ikifuatiwa na Magharibi B 166 (12.9%) na Kaskazini A 130 (10.1%). Wilaya ya Kusini, Kaskazini B, na Micheweni ziliripoti idadi ndogo ya vifo vilivyosajiliwa ambavyo ni chini ya 40 kila moja.

Aidha, usajili wa vifo umeonekana kupungua kwa kipindi cha Januari - Machi 2025 na kufikia vifo 668 kutoka vifo vilivyosajiliwa 1,287 kwa kipindi cha Oktoba -Disemba 2024, sawa na upungufu wa asilimia 48.1. Wilaya zinazoonesha upungufu zaidi wa usajili wa vifo, ni Mjini kutoka vifo 633 hadi vifo 211, Wilaya ya Kaskazini A kutoka vifo 130 hadi vifo 38, na Wilaya ya Magharibi B kutoka vifo 166 hadi vifo 125.

Aidha Wilaya ya Kusini iliripoti ongezeko la usajili wa vifo 17 hadi vifo 31 kwa kipindi cha (Oktoba - Disemba 2024) hadi (Jan-Machi, 2025). Hali hii inawekana kuwa inatokana

na kuwa na uwelewa mdogo wa jamii juu ya usajili wa vifo vinavyotokea katika jamii, juhudi zaidi za uhamasishaji kwa jamii unahitajika.

**Jadweli Na. 5: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Okt -Dis, 2024 na Jan-Machi 2025**

| Wilaya | Oktoba - Disemba 2024 | | | Jan-Machi, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 75 | 55 | 130 | 26 | 12 | 38 |
| Kaskazini B | 12 | 3 | 15 | 8 | 7 | 15 |
| Kati | 17 | 16 | 33 | 20 | 10 | 30 |
| Kusini | 7 | 10 | 17 | 15 | 16 | 31 |
| Mjini | 352 | 281 | 633 | 109 | 102 | 211 |
| Magharibi A | 26 | 24 | 50 | 25 | 19 | 44 |
| Magharibi B | 92 | 74 | 166 | 68 | 57 | 125 |
| Micheweni | 27 | 8 | 35 | 25 | 9 | 34 |
| Chakechake | 46 | 18 | 64 | 30 | 18 | 48 |
| Wete | 70 | 19 | 89 | 30 | 21 | 51 |
| Mkoani | 36 | 19 | 55 | 28 | 13 | 41 |
| **Jumla** | **760** | **527** | 1,287 | 384 | 284 | 668 |

## 2.2.2 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Jan-Machi, 2024 na Jan-Machi, 2025

Katika kipindi cha Januari - March 2024, usajili wa vifo ulikuwa wa kiwango cha juu kwa jumla ya vifo 1,555, huku wanaume wakiwa 863 na wanawake 692. Kwa upande wa Januari - Machi 2025, usajili wa vifo, ulishuka ikilinganishwa na robo mwaka kama hiyo katika mwaka 2024 ambapo jumla ya vifo 668 vilisajiliwa, ikiwa ni sawa na upungufu wa vifo 887.

Upungufu huo zaidi umeonekana katika wilaya ya Mjini ambapo usajili umeshuka kutoka vifo 916 kwa Jan-Machi, 2024 na kushuka hadi vizazi 211 kwa Jan-Machi, 2025. Hali hii inaashiria kuwa na uelewa mdogo wa jamii juu ya usajili wa matukio ya kijamii hususan usajili wa vifo.

**Jadweli Na. 6: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Jan -Machi, 2024 na Jan-Machi 2025**

| Wilaya | Jan-Machi, 2024 | | | Jan-Machi, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 72 | 55 | 127 | 26 | 12 | 38 |
| Kaskazini B | 17 | 8 | 25 | 8 | 7 | 15 |
| Kati | 16 | 10 | 26 | 20 | 10 | 30 |
| Kusini | 13 | 17 | 30 | 15 | 16 | 31 |
| Mjini | 509 | 407 | 916 | 109 | 102 | 211 |
| Magharibi A | 67 | 52 | 119 | 25 | 19 | 44 |
| Magharibi B | 40 | 58 | 98 | 68 | 57 | 125 |
| Micheweni | 32 | 5 | 37 | 25 | 9 | 34 |
| Chakechake | 32 | 33 | 65 | 30 | 18 | 48 |
| Mkoani | 19 | 12 | 31 | 30 | 21 | 51 |
| Wete | 46 | 35 | 81 | 28 | 13 | 41 |
| **Jumla** | 863 | 692 | 1,555 | 384 | 284 | 668 |

## 2.3 Usajili wa Ndoa

Jumla ya Ndoa 3,994 zimesajiliwa kwa kipindi cha Januari – Machi, 2025, jumla ya ndoa 1,308 zimefungwa na kusajiliwa mwezi wa Januari 2025, na kuongezeka hadi kufikia ndoa 1,623 mwezi Febuari, 2025 na kupungua hadi kufikia ndoa 1,063 zilizosajiliwa kwa mwezi wa Machi 2025 (Jadweli Na. 5).

Aidha, takwimu zinaonesha kuwa Wilaya ya Kaskazini A imesajii ndoa 1,006 (25.1%), ikifuatia na wilaya ya Kati na Mjini ambazo zimeripoti kusajili ndoa 762 (19.1%) na 610 (15.3%) mtawalia. Bado kuna mwamko mdogo wa usajili wa ndoa ukilinganisha na ndoa zinazofungwa katika jamii, aidha kwa kipindi cha Januari – Machi 2025 Wilaya ya Mkoani na Wilaya ya Micheweni zimesajili idadi ndogo ya ndoa 15 (0.4%) na 26 (0.7%) mtawalia.

**Jadweli Na. 7: Usajili wa Ndoa kwa Wilaya, Januari – Machi 2025**

| Wilaya | Jan-2025 | Feb-2025 | Mac-2025 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 145 | 345 | 516 | 1,006 |
| Kaskazini B | 49 | 228 | 17 | 294 |
| Kati | 67 | 445 | 250 | 762 |
| Kusini | 93 | 55 | 46 | 194 |
| Mjini | 431 | 157 | 22 | 610 |
| Magharibi A | 170 | 127 | 15 | 312 |
| Magharibi B | 248 | 124 | 111 | 483 |
| Micheweni | 21 | 1 | 4 | 26 |
| Chakechake | 75 | 125 | 50 | 250 |
| Mkoani | - | 8 | 7 | 15 |
| Wete | 9 | 8 | 25 | 42 |
| Jumla | 1,308 | 1,623 | 1,063 | 3,994 |

## 2.4 Usajili wa Talaka

Jumla ya Talaka 383 zimesajiliwa kwa kipindi cha Januari–Machi, 2025. Jumla ya talaka 137 (35.8%) zimesajiliwa Januari 2025, na kuongezeka hadi talaka 181 (47.3%) kwa mwezi Febuari 2025, aidha mwezi Machi 2025 usajili wa talaka umepungua hadi kufikia talaka 65 (17.0%) mwezi Machi 2025 (Jadweli Na. 6).

Aidha, Wilaya ya Kati na Mjini zimeripoti idadi kubwa zaidi ya talaka ikilinganishwa na Wilaya nyingine kila moja imesajili jumla ya talaka 85 (22.2%) kwa kipindi cha Januari-Machi 2025 zikifuatiwa na Wilaya ya Kaskazini A imeripoti kusajili ndoa 77 (20.1%). Bado kuna mwamko mdogo wa usajili wa talaka kwa jamii, hali hii inaonekana kuwa kubwa zaidi katika Wilaya ya Micheweni na Wete ambazo hazikuwa na usajili kabisa wa talaka katika kipindi cha Januari-Machi 2025.

**Jadweli Na. 8: Usajili wa Talaka kwa Mwezi, Januari - Machi 2025**

| Wilaya | Jan-2025 | Feb-2025 | Mac-2025 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 7 | 62 | 8 | 77 |
| Kaskazini B | 2 | 15 | 0 | 17 |
| Kati | 14 | 43 | 28 | 85 |
| Kusini | 9 | 11 | 8 | 28 |
| Mjini | 72 | 11 | 2 | 85 |
| Magharibi A | 10 | 3 | 0 | 13 |
| Magharibi B | 23 | 9 | 19 | 51 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 25 | 0 | 25 |
| Mkoani | 0 | 2 | 0 | 2 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | 137 | 181 | 65 | 383 |

## 3.0 Hitimisho

Kwa ujumla, taarifa za matukio ya kijamii ni muhimu sana kwa kuimarisha huduma za kijamii, kuleta mabadiliko chanya, na kukuza ustawi wa jamii. Jamii inapaswa kushiriki kikamilifu katika kusajili matukio ya kijamii kwa maendeleo ya Taifa.

Ikumbukwe kuwa takwimu zilizowasilishwa hapa ni zile tu zilizosajiliwa rasmi kupitia Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA). Kuna matukio mengi kwenye jamii hasa ya vifo na talaka ambayo yanatokea katika jamii na hayasajiliwi rasmi. Aidha, jamii inasisitizwa kuwa na utamaduni wa kusajili matukio ya Kijamii kwa mamlaka husika ili yaweze kusajiliwa, na kuisaidia serikali na wadau wengine wa maendeleo katika kupanga mipango yenye tija kwa taifa.

## Maelezo Muhimu

- Kizazi hai ni tukio la mtoto kuzaliwa akiwa hai, yaani, mtoto ambaye amezaliwa ana pumzi, anafanya harakati, na ana ishara za maisha. Kizazi hai mara nyingi hufuatana na mchakato wa kawaida wa kujifungua, ambapo mtoto huzaliwa kuja ulimwenguni.

- Kifo ni tukio la mwisho la kuishi. Ni tukio ambalo mwili huacha kabisa kufanya kazi kwa binadamu, kifo hutokea wakati moyo unasimama na kusitisha mtiririko wa damu mwilini, na ubongo kusimama kufanya kazi.

- Sheria Namba 3 ya 2018, inaeleza kuwa Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) ina majukumu ya kusajili Matukio ya kijamii na kutoa vyeti maalum, matukio hayo ni Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na Wasiokua Wazanzibari Wakaazi.

- Sheria Namba 9 ya mwaka 2007 inaeleza kuwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa

Serikali, Zanzibar ina mamlaka ya kuratibu na kusimamia uendeshaji wa kazi za takwimu katika taasisi zote za Serikali na binafsi zinazofanya shughuli zake hapa Zanzibar.

***Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:***


**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI,**
S.L.P 2321, 7 Barabara ya Fumba, 71125 Mjini Magharibi,
Zanzibar – Tanzania.
Simu  +255 24 2231869
Faksi: +255 24 2231742
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: www.ocgs.go.tz

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMI**
Simu: +255 772 400 597
S.L.P: 264
Barua pepe: info@zcsra.go.tz
Flamingo, Migombani Zanzibar Tanzania.